



MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na.23. Msimu wa Kilimo 2022/23

Tathmini ya Mei 11-20, 2023 na Matazamo kwa Kipindi cha Mei 21-31, 2023

MUHTASARI


- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi yanayopata mvua za Msimu inatarajiwa kusaidia kukomaa kwa mazao hususan mahindi na mpunga.
- Kupungua kwa unyevunyevu kwenye udongo kunatarajiwa kuathiri ukuaji wa mazao hususan katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2023

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika wakati ile kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu. Hali hii ilipelekea kuusukuma ukanda mvua (ITCZ) katika maeneo ya Kaskazini mwa nchi. Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikua la wastani hadi juu kidogo ya wastani, na hivyo kuwa na mchango mdogo katika kusafirisha hewa yenye unyevunyevu kuvuma kuelekea ukanda wa pwani ya nchi. Katika eneo la tropiki ya kati ya bahari ya Pasifiki joto la bahari lilikua la juu kidogo ya wastani. Kwa upande mwingine, joto la bahari katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola) lilikua la juu ya wastani na hivyo kuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi.

TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2023

Katika kipindi hiki maeneo mengi nchini yalipata mvua chini ya milimita 10 isipokuwa maeneo machache ya mikoa ya Pwani na Lindi ambayo yalipata mvua zaidi ya milimita 250 kama inavyoonekana katika Kielelezo.



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Mei 11-20, 2023

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2023

Mvuua zilizonyesha katika dekadhi hii, zimesaidia ukuaji na maendeleo ya mazao katika maeneo yanayopata mvua za masika. Hali ya ukavu iliyojitokeza hususan katika maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka ilisaidia kukomaa kwa mahindi na mpunga. Hali hii pia ilisaidia shughuli za uvunaji wa mpunga hususan katika mikoa ya Tabora na Mbeya.

Kwa ujumla, zao la mahindi na mpunga lipo katika hali nzuri hususan kwenye maeneo yanayopata mvua za msimu. Maeneo yanayopata mvua za masika hususan katika mikoa ya Mwanza, Simiyu, Mara, Kagera, Morogoro, Arusha, na Pwani mahindi yapo katika hatua ya kutoa mbelewele, na yanaendelea vizuri.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo ulikuwa wa kuridhisha katika maeneo mengi nchini kutokana na mvua zinazoendelea.

**HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA
MEI 11-20, 2023**

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito na mabonde kilikuwa cha kawaida katika maeneo mengi nchini.

**MIFUMO YA HALI YA HEWA
INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA
MEI 21-31, 2023**

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kuuruhusu ukanda mvua (ITCZ) kuelekea kaskazini zaidi mwa nchi. Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani, hali hii inatarajiwa kuwa na mchango mdogo katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya pwani. Katika eneo la tropiki ya kati ya bahari ya Pasifiki joto la bahari linatarajiwa kuwa la wastani. Kwa upande mwingine, joto la bahari katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la juu ya wastani na hivyo kuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi.

**HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA MEI 21-31, 2023**

Maeneo ya kanda ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kupata mvua na ngurumo za radi.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi kwa baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), magharibi mwa

nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Niombe na Iringa). Pwani va kusini (mikoa ya

**HALI YA HEWA KILIMO:
MATARAJIO NA USHAURI KATIKA
KIPINDI CHA MEI 21-31, 2023**

H

ali ya ukavu inayotarajiwa hususan katika maeneno yanayopata mvua za Msimu itasaidia katika kukomaa kwa mahindi na mpunga. Hata hivyo hali hii inaweza kuathiri maendeleo ya mahindi yaliyo katika hatua ya kutoa mbelewele hususan katika maeneo yanayopata mvua za masika.

Kupungua kwa unyevunyevu kwenye udongo kunatarajiwa kuathiri ukuaji wa mazao hususan katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa.

Wakulima na maafisa ugani wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao mashambani ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kutokana na mlipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza hususan kwa maeneo yanayopata mvua za masika.

Jamii za wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye bahari ya Hindi na maziwa makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi. Wafugaji pia wanashauriwa kuhakikisha mifugo yao inalindwa dhidi ya hali mbaya ya hewa na magonjwa ya mlipuko.

Kwa ujumla, inashauriwa kuzingatia utabiri wa hali ya hewa katika shughuli na mipango ya kila siku.

**HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA MEI 21-31, 2023**

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya kawaida. Hata hivyo, jamii inashauriwa kuhifadhi maji ili kuepuka upungufu unaoweza kujitokeza hapo baadae.